



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



03/04/2025

Kumb Na. LMC/F.30/2/01

Mkurugenzi Mtendaji
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
SLP 938
Dar es Salaam

**YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED
(VCSL)**

Rejea somo tajwa hapo juu.

1. Naitambulisha kwako kampuni tajwa hapo juu, ambayo inamalengo ya kuwezesha vijiji mbalimbali hapa Tanzania kutekeleza biashara ya Kaboni kupitia mfumo unaojulikana kama "Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na ukataji miti hovy na uharibifu wa misitu" (MKUHUMI).
2. Mpango huu unasaidia utunzaji wa Misitu ya Asili inayomilikiwa na Vijiji, kwa mujibu wa Vifungu namba 4 (c) (i), 32 (1) (a) na (b) na 35 (6) (b) vya Sheria ya Misitu sura ya 323 ya Sheria za Tanzania.
3. VCSL inashirikiana na vijiji na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kutekeleza MKUHUMI, kwalengo la kuzalisha na kuuza krediti za Kaboni, ambapo vijiji vitapata fedha zitakazo saidia maendeleo ya jamii hususani kuboresha kilimo, elimu ya sekondari na ufundi, afya, maji na upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.
4. Mradi wa VCSL inajulikana kama *Village Climate Solutions Project (VCSP)* na umesajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mfumo wa Kimataifa wa Viwango vya Kaboni (*Verified Carbon Standards - VCS*) na Viwango vya Ubora (*Climate, Community and Biodiversity – CCB standards*) kupitia akaunti namba 1325.
5. Katika Wilaya yetu, Mradi huu unatekelezwa katika vijiji/Mitaa ifuatavyo (Ramani imeambatishwa)
 - i) Ruhoma
 - ii) Kinyope
 - iii) Milola Magharibi
 - iv) Kiwawa
 - v) Muungano
 - vi) Mkombamosi
 - vii) Makumba
 - viii) Likwaya
 - ix) Namkongo
 - x) Mputwa
 - xi) Nandambi
 - xii) Mkanga1

6. Tunawaomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kushirikiana na kampuni hii katika masuala yote yanayohusiana na uwekezaji na utekelezaji wa mradi huu ili kuhakikisha mafanikio yake na manufaa kwa jamii.
7. Tunatanguliza shukrani zetu kwa ushirikiano wako.

Wako katika utumishi,



STANFORD MWAKATAGE

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA
LINDI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

Kiambatisho: Ramani kuonesha eneo la Mradi katika Manispaa ya Lindi

